

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



“MET Opp. Maweni
Hospital,
S.L.P. 880,
47115 KIGOMA,
Barua Pepe: rbckigoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

KIGOMA - APRILI 28, 2020

TAARIFA KWA UMMA
KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

KARANI WA MAHAKAMA YA MWANZO MWANDIGA KUFIKISHWA
MAHAKAMANI KWA KOSA LA KUOMBA NA KUPOKEA RUSHWA YA
SHILINGI 170,000/=

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (**TAKUKURU**) Mkoa wa Kigoma Leo Aprili 28, 2020 itamfikisha katika Mahakama ya Wilaya Kigoma Bw. **JACKSON MREFU** (58) ambaye ni mhudumu wa Mahakama ya Mwanzo Mwandiga kwa kosa la kuomba na kupokea kiasi cha Shilingi laki moja na elfu sabini kutoka kwa **IMELDA DOSHA** mteja aliyefika Mahakamani hapo kwa ajili ya kufungua kesi ya Madai.

Uchunguzi wa **TAKUKURU** Mkoa wa Kigoma ulibaini kwamba, Bw. **JACKSON MREFU** akiwa ni mtumishi wa Mahakama ya mwanzo Mwandiga, mnamo tarehe 19/09/2019 akiwa katika utekelezaji wa majukumu ya mwajiri, alishawishi kupewa kiasi cha shilingi 170,000/= kutoka kwa **IMELDA DOSHA** kama sharti la kufungua kesi ya madai kutokana na malalamiko yaliyofikishwa mahakamani hapo na mteja husika

Aidha Bw. Jackson Mrefu alipokea fedha aliyoiomba kiasi cha Shilingi 170,000/= kutoka kwa **IMELDA DOSHA** kwa awamu tofauti tofauti ambapo tarehe 19/9/2019 alipokea shilingi 30,000/=, tarehe 20/9/2019 alipokea Shilingi 60,000/=, tarehe 25/9/2019 alipokea kiasi cha shilingi 70,000/= na tarehe 26/9/2019 aliweza kupokea shilingi 11,000 kwa njia ya Mpesa ili kutimiza kiasi cha shilingi 170,000/= kiasi cha fedha alichokuwa ameomba ili kutimiza sharti la kufungua kesi.

Vitendo hivi ni makosa chini ya Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007.

Katika hatua nyingine, mnamo tarehe 25/04/2019 Bw. **JACKSON MREFU** aliweza kufungua kesi ya Madai Na. 45/2019 katika Mahakama ya Mwanzo mwandiga iliyomhusu **IMELDA DOSHA** dhidi ya **CHRISTINA**, baada ya kuwa amepokea hongo ya shilingi 160,000/= kutoka kwa **IMELDA DOSHA**. Aidha Bw. **JACKSON** baada ya kufungua kesi aliendelea kushawishi kupewa sh 10,000 iliyokuwa imebaki ili kukamilisha fedha kiasi cha sh 170,000/= alizokuwa ameomba, ambapo mnamo tarehe 26/04/2019 fedha kiasi cha Shilingi 11,000/= ziliweza kutumwa kwa njia ya **M-PESA** kwenye simu yake Na.**0767491218**, shilingi 1,000/= ikiwa ni gharama ya kutoa fedha hiyo.

TAKUKURU mkoa wa Kigoma inatoa wito kwa watumishi wote wa Umma kuepuka kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kazi.

Watumishi wote wa Serikali, Mashirika ya Umma, Taasisi za Umma na binafsi wanahimizwa kuacha tabia ya kuomba au kukubali kupokea manufaa yoyote kutoka kwa mtu wanayemhudumia au wanaye tarajia kumhudumia kwani kwa kufanya hivyo wanatenda makosa dhidi ya rushwa.

Ifahamike kuwa watumishi wanalipwa mishahara na Serikali ambayo inatokana na kodi za wananchi wanaowahudumia. Hivyo kila mtumishi lazima ajue kuwa anao wajibu wa kutekeleza majukumu ya mwajiri kwa uadilifu huku akifuata na kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kazi na siyo kufanya kazi kwa misingi ya rushwa na upendeleo.

TAKUKURU Mkoa wa Kigoma haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria watumishi wa Umma na Taasisi binafsi au watu wengine wasiotaka kubadilika, na wanaoendelea kukumbatia vitendo vya rushwa.

Imetolewa na:

Nestory Gatahwa

**KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M)
KIGOMA**